

**MKATABA WA UPANGISHAJI ARDHI**

**KATI YA**

**CHUNYA & SONGWE ENERGY LIMITED**

**NA**

**SERIKALI YA KIJJI CHA GUA**

## **MKATABA WA UPANGISHAJI WA ARDHI**

MKATABA HUU UMEFANYIKA leo tarehe 14.....Mwezi .....02. 2025

**KATI YA**

**CHUNYA & SONGWE ENERGY LIMITED** wa S.L.P 5823, Dar es Salaam (ambaye ndani ya mkataba huu atajulikana kama "Mpangaji") wa upande mmoja.

**NA**

**SERIKALI YA KIJIKI CHA GUA** wa S.L.P 35, Mkwajuni Songwe (ambaye ndani ya mkataba huu atajulikana kama "") kwa upande mwingine.

**KWAMBA** Mwenye ardhi ni mmiliki halali wa Ardhi iliyopo kijiji cha Gua , Mkwajuni Songwe Tanzania.

**NA KWAMBA** Mwenye ardhi ameamua kwa hiyari yake kumpangisha Mpangaji ardhi hiyo yake kwa ajiri ya shughuli ya uzalishaji wa umeme na Mpangaji yuko radhi kupanga ardhi hiyo.

**HIVYO BASI MKATABA HUU NI UNASHUHUDI YAFUATAYO;**

1. Kwamba kodi (Malipo) ya upangaji wa ardhi yatakuwa kuchangia maendeleo ya kijiji kama ya fuatayo;
  - I. Cement 100
  - II. Bati 20 G.28 F.10
  - III. Eneo hilo lipo kitongoji cha Manda Juu (Tulileni) lenye ukubwa wa ekali Thelathini (30).
2. Kipindi cha mkataba itakuwa ni miaka thelathini na tatu (33).
3. Kwamba kwa kutia sahihi mkataba huu Mwenye ardhi anakiri makubaliano tajwa hapo juu.
4. Mpangaji anakiri kutumia ardhi hiyo kwa shughuli halali za uzalishaji wa umeme na si vinginevyo au shughuli halali yanayoruhusiwa na kutambulika kisheria tu.
5. Mpangaji haruhusiwi kumpangisha mtu mwingine yeyote bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mwenye ardhi.
6. Pande zote mbili zinaelewana kwamba katika muda wa makubaliano ya upangaji humu, mpangaji atakuwa na haki ya kipekee ya kununua ardhi iliyokodishwa na atakuwa na haki ya kushughulikia upataji wa Haki Inayopewa ya Kumiliki. Imekubaliwa zaidi kuwa mwenye nyumba atawajibika kutekeleza hati zinazohitajika za kuhamisha, ikijumuisha makubaliano ya uuzaji kuhusiana na ardhi iliyokodishwa kwa kuzingatia masharti na masharti yatakayotolewa ama

kabla au baada ya kumalizika kwa muda wa kukodisha hapa mradi tu kodi yote inayostahili wakati wa uhamisho itakuwa imelipwa kikamilifu.

7. Mpangaji ataruhusiwa kufanya maendeleo ya ardhi ili kuwezesha maendeleo ya mradi mfano kujenga ofisi, kusimika nguzo na kufanya ukatuuaji ili kuwezesha vyuma kusimama.
8. Mkataba huu unanza rasmi tarehe 14 Mwezi 02, 2025 .
9. Kwamba mpangaji atajitegemea mwenyewe kwenye suala la Ulinzi, na gharama hizo hazitomhusu mwenye adhi.
10. Kwamba mpangaji atatakiwa kuweka maeneo yote yanayoizunguka ardhi katika hali ya usafi na mandhari nzuri kwa kipindi chote cha upangaji.
11. Kwamba kama mpangaji atataka kuendelea na Mkataba huu kwa kipindi kingine basi atatakiwa kutoa notisi miezi mitatu (3) kabla ya mkataba huu kufika kikomo.
12. Endapo kutatokea mgogoro kati ya mpangaji na mwenye ardhi, mgogoro huo utasuluhishwa baina yao kama suluhu haitapatikana, mgogoro huo utawasilishwa kwenye baraza la ardhi na kufuata utaratibu wa kawaida wa sheria baada ya hapo. Sheria hizo zitakuwa za Tanzania.
13. Mpangaji atahakikisha hafanyi shughuli zozote za uharibifu wa mazingira na ataitunza ardhi hiyo vizuri lengo likiwa HATAFANYA UARIBIFU WAMAZINGIRA.
14. Kwamba mtu yeyote baina ya pande hizi mbili atakayekiuka masharti mwenzake anayo haki ya kufungua shitaka dhidi ya upande wa pili kwautaratibu wa mkataba huu uliohainishwa hapo kwenye kifungu cha 12.
15. Kwamba mkataba huu unasimamiwa na sharia za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**KWA USHUHUDA** wa makubaliano hayo pande zote mbili zimetia sahihi kama ilivyo hapa chini;

Kwa niaba ya SERIKALI YA KIJIKI CHA GUA  
JINA ALFRED JORDAN MARIWA  
SAHIHI [Signature]  
WADHIFA MWENYEKITI KJI - GUA  
TAREHE 14/02/2025



Kwa niaba ya CHUNYA & SONGWE ENERGY LIMITED (SPV)  
JINA DANIEL ELIAKIM MWAKYOMA  
SAHIHI [Signature]  
WADHIFA MKURURUGENZI MKUU  
TAREHE 17/02/2025



Leo Tarehe...14.....Mwezi...02..... 2025

MBELE YANGU:

[Signature]



KAMISHNA WA KIAPO



19M

Certified true copy